**Issue no:** 01 | **Vol no:** 07 | **June** 2026: 26-34

# Aina za Urejelezi katika Gazeti la *Taifa Leo*: Mtazamo wa Kipragmatiki

**Simon Kipkoech Kirui**

Bomet University, Kenya.
Main author email: kiruisymmo@gmail.com

**Article History**
Received: **2026.04.19**
Accepted: **2026.05.17**
Published: **2026.06.22**

**Cite this article in APA**
Kirui, S. K. (2026). Aina za urejelezi katika gazeti la *Taifa Leo*: Mtazamo wa kipragmatiki. *Editon consortium journal of kiswahili*, *7*(1), 26-34. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v7i1.713

**Ikisiri**
Makala hii inabainisha aina za urejelezi katika gazeti la *Taifa Leo* na jinsi zinavyochangia kuleta mshikamano katika matini. Suala la urejelezi limechunguzwa na wasomi wengi. Hata hivyo, hakuna utafiti ambao umefanywa kwa kina kuhusu aina za urejelezi katika gazeti la *Taifa Leo*. Makala hii iliongozwa na Nadharia ya Sarufi Amilifu iliyoendelezwa na Halliday (1985, 1994, 1999), Halliday na Matthiessen (2004) na Matthiessen (2013) kwa kuangazia mtazamo wa Halliday na Hasan (1976). Aidha, Nadharia ya Uhusiano iliyoasisiwa na Wilson (2003) na Wilson na Sperber (2002) ilitumika kama nadharia changizi katika kufafanua jinsi wasomaji wanavyofikia maana tambuzi katika matini. Mbinu ya makala hii ni ya kimaelezo. Sampuli ya utafiti ilikuwa ya kimakusudi, ambapo nakala 30 za *Habari za Kaunti* zilizo na aina mbalimbali za urejelezi zilichaguliwa. Data iliyotumika katika makala hii ilikusanywa kutoka gazeti la *Taifa Leo* kati ya mwezi wa Juni na Julai 2020 kwa ajili ya tasnifu ya uzamili iliyoshughulikia suala la Urejelezi katika Gazeti la *Taifa Leo*: Mtazamo wa Kipragmatiki. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa ili kubainisha aina za urejelezi katika gazeti la *Taifa Leo* na jinsi zilivyotumika kuleta mshikamano katika matini. Matokeo yameonyesha kuwa aina mbalimbali za urejelezi zimetumika kuleta mshikamano katika matini. Makala hii inaonyesha kuwa urejelezi wa kiendofora, urejelezi nafsi, urejelezi wa kuashiria na urejelezi wa kulinganisha umetumika katika *Habari za Kaunti* ili kuleta mshikamano katika matini. Data ya makala hii imewasilishwa kwa kutumia maelezo ili kuonyesha jinsi aina mbalimbali za urejelezi zinavyochangia kuleta mshikamano katika matini. Utafiti huu utawafaa wasomaji wa gazeti katika kutambua na kufasiri aina mbalimbali za urejelezi kwa njia inayofaa ili kupata habari iliyokusudiwa na mwandishi.

**Key words**: Anafora, katafora, mshikamano, uhusiano, urejelezi.

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## UTANGULIZI

Ingawa suala la urejelezi ni kiungo muhimu katika ujenzi wa matini, hadi sasa kuna tafiti chache zinazozamia suala hili hususan katika gazeti la *Taifa Leo*. Utafiti huu unalenga kuziba pengo hili kwa kubainisha aina za urejelezi katika gazeti la *Taifa Leo* na namna zinavyosaidia kujenga matini na kufanikisha mawasiliano ya kimaana. Ili ujumbe uwafikie wasomaji wa gazeti, ni sharti sentensi ziwe na mshikamano. Sentensi ambazo hazina mshikamano huwatatanisha wasomaji na hivyo kufanya ujumbe usifasiriwe kwa urahisi. Makala hii inashughulikia aina za urejelezi katika gazeti la *Taifa Leo* na jinsi zinavyochangia kuleta mshikamano katika matini.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Kulingana na Halliday na Matthiessen (2004), urejelezi ni ufasiri wa kipashio kimoja kisemantiki kupitia kwa kurejelea kipashio kingine katika matini. Suala la urejelezi limeshughulikiwa na wasomi kama vile Sukthanker et al. (2020), Habarkah (2019), Khofidoh (2017), Saddimbah (2011) na Schubert (2008). Isitoshe, suala la uhusiano limeshughulikiwa na wasomi kama vile Toews (2016) na Ojode (2014).

Sukthanker et al. (2020) wanafafanua aina mbalimbali za urejelezi. Ufafanuzi wao ulitoa mwelekeo muhimu kuhusu namna ya kufasiri maana ya viwakilishi vinavyorejelea nomino moja au zaidi katika matini. Japo utafiti huo umejikita katika matumizi ya urejelezi katika tafsiri, ulichangia katika kutambua aina za urejelezi katika *Habari za Kaunti*.

Habarkah (2019) anafafanua kuwa urejelezi huchangia katika kuleta mshikamano katika matini. Utafiti huo ulikusanya data kutoka barua na ulichangia katika kutambua aina mbalimbali za urejelezi katika *Habari za Kaunti*. Khofidoh (2017) anaeleza kuwa urejelezi ni muhimu katika kuleta mshikamano katika matini. Kulingana naye, matini iliyo na mshikamano hueleweka kwa urahisi. Utafiti huo ulitumia nadharia tofauti na utafiti huu, lakini ulichangia katika kufafanua vipengele vilivyochunguzwa katika utafiti huu.

Saddimbah (2011) anaeleza kuwa vijenzi mbalimbali vya mshikamano huchangia kuleta muwala katika matini. Utafiti huo ulitumia nadharia tofauti na utafiti huu, lakini ulichangia katika kuonyesha jinsi urejelezi unavyochangia kuleta mshikamano katika matini.

Schubert (2008) anasema kuwa urejelezi wa kianafora ni muhimu katika kutambua kitu au jambo linalorejelewa katika matini. Maelezo haya yalisaidia katika kutambua kitajwa kilicho nyuma ya sentensi moja au zaidi kwa kutumia anafora. Maelezo ya Schubert yalichangia katika kutambua aina mbalimbali za urejelezi katika *Habari za Kaunti*.

Toews (2016) anafafanua kuwa nadharia ya Uhusiano ni nadharia ya kitambuzi ya mawasiliano ambayo inaweza kutumika kufasiri maana ya eksplisiti na implisiti. Isitoshe, anaeleza kuwa ili mawasiliano yafanikiwe, msemaji anafaa kutoa vidokezo vinavyovuta makini ya msikilizaji kwa jambo muhimu linalozungumziwa. Maelezo haya yalichangia katika kutambua mihimili ya nadharia ya Uhusiano.

Ojode (2014) anafafanua kuwa nadharia ya Uhusiano ni muhimu katika kutambua maana iliyokusudiwa na mwimbaji katika nyimbo zake. Kulingana naye, msikilizaji wa nyimbo anaweza kufikia maana zilizokusudiwa na mwimbaji kupitia vidokezo, tajriba ya msikilizaji na muktadha. Maelezo haya yalichangia katika uelewa wa maana ya kauli mbalimbali zilizotumika katika *Habari za Kaunti*. Isitoshe, utafiti huo ulichangia kubainisha jinsi urejelezi wa kiakili unaweza kutumika kuleta mshikamano kupitia urejelezi wa muktadha, ufahamu wa awali na kiwango cha uhusiano.

### Msingi wa Nadharia

Makala hii imeongozwa na nadharia mbili katika kuchanganua data. Nadharia ya Sarufi Amilifu iliyoendelezwa na Halliday (1985, 1994, 1999), Halliday na Matthiessen (2004) na Matthiessen (2013) kwa kuangazia mtazamo wa Halliday na Hasan (1976). Nadharia hii ilitumika kutathmini iwapo mhimili wa maana katika matini unaweza kutumiwa kiurejelezi katika *Habari za Kaunti* ili kuleta mshikamano katika matini. Aidha, Nadharia ya Uhusiano iliyoendelezwa na Carson (2002), Wilson na Sperber (2002) na Wilson (2003) ilitumika katika utafiti huu kutathmini iwapo mihimili ya kanuni tambuzi na kanuni za mawasiliano inaweza kutumiwa kiurejelezi ili kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*.

### Mihimili ya Nadharia ya Sarufi Amilifu

#### Maana Tambuzi

Maana tambuzi ni uwezo wa mzungumzaji kuelewa mambo kwa kutumia lugha kueleza mambo yanayotendeka katika ulimwengu wa kawaida na katika

fikra zake. Mhimili wa maana tambuzi ulitumika kutathmini jinsi waandishi wa *Habari za Kaunti* hutumia lugha kueleza mambo yanayotendeka katika ulimwengu halisi na tajriba zao kwa kutumia sentensi au aya zenye mshikamano.

**Maana Husishi**

Maana husishi huhusika na kutumia lugha kuleta utangamano katika jamii. Mhimili huu haukuhusishwa katika utafiti huu.

**Maana Matini**

Maana matini ni jinsi yale tunayosema yameshikana pamoja na kuhusiana na kilichosemwa hapo awali na kulingana na muktadha unaotuzunguka. Mhimili huu ulitumika kutathmini jinsi waandishi wa *Habari za Kaunti* hutumia urejelezi kuunganisha maana kutoka sentensi au aya moja hadi nyingine ili kuleta mshikamano katika matini.

**Mihimili ya Nadharia ya Uhusiano**

**Kanuni Tambuzi**

Katika kanuni tambuzi, msemaji anahitajika kutoa kauli ambazo zinaeleweka kwa msikilizaji kwa urahisi. Msemaji huchochea akili ya msikilizaji kwa kutumia vidokezi vinavyomfanya msikilizaji kuteka makini yake tu katika ujumbe muhimu na kufahamu ujumbe unaolengwa na msemaji kwa urahisi. Mhimili huu ulitumika kutathmini iwapo kauli zinaweza kutumiwa kiurejelezi ili kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*.

**Kanuni Mawasiliano**

Mhimili wa kanuni mawasiliano unahusiana na kutumia lugha yenye usemi mkubwa wa uhusiano katika kila tendo la mawasiliano. Msemaji anafaa kutumia lugha yenye kiwango kikubwa cha uhusiano. Mhimili huu huongoza utaratibu wa kuchakata na kufasiri ujumbe kwa kuzingatia kiwango cha uhusiano. Katika mhimili huu, muktadha ambamo kauli imetolewa huchangia katika ufahamu wa maana katika kauli ya msemaji. Mhimili huu ulitumika katika urejelezi wa muktadha katika matini ili kupata maana iliyokusudiwa na msemaji au mwandishi.

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaelezo. Hivyo, data zilizotumika si za takwimu. Data zilizotumika katika makala hii zilikusanywa kutoka *Habari za Kaunti* katika gazeti la *Taifa Leo*. *Habari za Kaunti* za mwezi wa Juni 2020 hadi Julai 2020 zilisomwa ili kupata data ya utafiti huu. Nakala 61 za *Habari za Kaunti* katika gazeti la *Taifa Leo* zilikusanywa kwa muda wa miezi miwili. Miezi hii miwili ilitoa *Habari za Kaunti* zilizoandikwa na waandishi mbalimbali. *Habari za Kaunti* zilichunguzwa kwa sababu habari hizi huandikwa kila siku na waandishi mbalimbali nchini Kenya, hivyo zikatoa sampuli kubwa ya kutumika katika utafiti huu. Nakala zote 61 zilisomwa kisha nakala 30 zilichaguliwa kimakusudi. Nakala hizi 30 zilizoonyesha aina mbalimbali za urejelezi zilichaguliwa ili kupata data iliyosaidia kufikia lengo la makala hii. Vigezo vilivyotumika kuchagua nakala 30 za *Habari za Kaunti* ni usampulishaji wa kimakusudi, ambapo sampuli ilichaguliwa kulingana na jinsi waandishi wa habari walivyotumia urejelezi kuleta mshikamano katika matini.

Baada ya data kukusanywa, aina mbalimbali za urejelezi ziligawanywa katika vikundi vitatu: urejelezi nafsi, urejelezi wa kuashiria na urejelezi wa kulinganisha kulingana na vikundi vilivyofafanuliwa na Halliday na Hasan (1976). Mhimili wa maana matini wa Sarufi Amilifu ulitumika kubainisha jinsi urejelezi ulivyotumika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*. Mihimili ya kanuni tambuzi na kanuni mawasiliano ya nadharia ya Uhusiano ilitumika kuchanganua data ili kubainisha jinsi waandishi wa *Habari za Kaunti* hutoa ujumbe ulio na mshikamano kwa wasomaji wao kupitia urejelezi wa muktadha, ufahamu wa awali na kiwango cha uhusiano.

Ili kuhakikisha uhalali na uaminifu wa data wakati wa uchambuzi, *Habari za Kaunti* zilizoteuliwa ziliorodheshwa na tarehe ambazo habari hizi ziliandikwa katika gazeti la *Taifa Leo* zilinakiliwa ili ziweze kurejelewa na kuthibitisha ukweli wa data ya makala hii. Data ya utafiti huu iliwasilishwa kwa kutumia maelezo kuonyesha jinsi aina mbalimbali za urejelezi zinavyochangia kuleta mshikamano katika matini.

**MATOKEO NA MAJADILIANO**

**Aina za Urejelezi katika Gazeti la *Taifa Leo***

Urejelezi ni ufasiri wa kipashio kimoja kisemantiki kwa kurejelea kipashio kingine katika matini. Urejelezi umegawika katika sehemu mbili kutegemea uamilifu wake katika matini: urejelezi wa kieksofora na urejelezi wa kiendofora. Urejelezi wa kieksofora hutokea pale ambapo ufasiri wa kitajwa hutegemea nje ya muktadha. Kitajwa kinachorejelewa hakipatikani katika matini ila msomaji anahitajika kufasiri kitajwa hicho nje ya muktadha. Urejelezi huu hauchangii katika kuleta mshikamano katika matini.

**Urejelezi wa Kiendofora**
Urejelezi wa kiendofora ni aina ya urejelezi ambapo ufasiri wa maana ya kipashio unajikita katika matini. Mtu au kitu kinachorejelewa kinaweza kutambulika katika matini. Urejelezi huu huchangia katika kuleta mshikamano katika matini. Kuna aina mbili za urejelezi wa kiendofora: anafora na katafora.

**Anafora**
Anafora ni kipashio cha kiisimu kinachotumiwa kurejelea neno au kitu kilichokuwa kimetajwa katika matini. Neno linatumiwa kurejelea mtu au kitu kilichokuwa kimetajwa awali katika matini. Urejelezi wa kianafora umetumika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*, kwa mfano:

*"Serikali imejitetea kuhusu ubomoaji wa vibanda katika ufuo wa Jomo Kenyatta almaarufu kama Pirates, Kaunti ya Mombasa."*

> *Kwenye mahojiano na Taifa Leo, Naibu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Makavazi ya Kenya (NMK) eneo la Pwani, Bw. Athman Hussein alisema wanashirikiana na serikali ya kaunti pamoja na Wizara ya Utalii ili kuupa ufuo huo sura mpya, ifikie hadhi ya kimataifa.*
>
> *Tumekuwa na mipango hii tangu tupewe mamlaka ya kusimamia ufuo huo. Eneo lenyewe limekuwako na vibanda vingi vibovu na hata hali ya usalama haijakuwa ya kuridhisha na tunataka kubadilisha haya yote', akasema Bw. Hussein… (Mutheu, 2020).*

Katika mfano huu, kiwakilishi nafsi kiambata tu- katika neno *tumekuwa* kinarejelea Mamlaka ya Makavazi ya Kenya na serikali ya Kaunti ya Mombasa ambazo zilikuwa zimetajwa katika aya ya pili katika matini. Naibu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Makavazi ya Kenya eneo la Pwani, Bw. Hussein anarejelea kianafora Mamlaka ya Makavazi ya Kenya na serikali ya Kaunti ya Mombasa iliyotajwa katika aya iliyotangulia. Kiwakilishi nafsi kiambata tu- kimetumika kuleta mshikamano katika matini.

**Katafora**
Katafora ni matumizi ya kipashio cha kiisimu kuonyesha neno litakalotajwa katika matini. Katafora ni aina ya urejelezi ambayo hutegemea neno lililo mbele ya matini ili kufasiriwa. Katafora imetumika katika *Habari za Kaunti* ili kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

*"Wazee kutoka jamii ya Wakamba wamezidisha juhudi za kutaka Kiongozi wa Chama cha Wiper, Bw. Kalonzo Musyoka amrithi Rais Uhuru Kenyatta kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2022."*

> *Akiongea na wanahabari wakiwa Mwala, mwenyekiti wa baraza la wazee wa koo za jamii ya Wakamba Boniface Kilonzo alihimiza jamii hiyo kuendelea kuunga mkono azma ya Bw. Kalonzo akisema nafasi yake ya kuongoza nchi imekaribia (Muthini, 2020).*

Bw. Boniface Kilonzo amerejelewa kupitia kiwakilishi nafsi kiambata a- ambacho kinatokea katika neno *akiongea* mwanzoni mwa aya. Urejelezi unaojitokeza hapa ni urejelezi wa katafora kwa sababu kiwakilishi nafsi kiambata a- kimetumika kurejelea nomino Bw. Boniface Kilonzo itakayotajwa katika matini. Urejelezi wa katafora umetumika kuonyesha uhusiano wa kimaana katika matini.

Mwandishi ametumia mhimili wa maana tambuzi kuelezea juhudi za wazee kutoka jamii ya Wakamba za kuunga mkono azma ya Bw. Kalonzo Musyoka za kumrithi Rais Uhuru Kenyatta kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2022. Mwandishi ametumia neno jamii kwa njia isiyo wazi. Ili msomaji aweze kupata maana iliyokusudiwa na mwandishi, itambidi apanue maana ya neno jamii kutumia kikamusi cha utambuzi. Katika kikamusi hicho, chukulizi zifuatazo zitakuzwa katika akili ya msomaji:

(i) watu wenye asili moja
(ii) mkusanyiko wa watu au vitu

Chukulizi zilizoorodheshwa hapo juu zinarejelea neno jamii kwa jumla na zimehifadhiwa katika akili ya mwandishi na msomaji. Msomaji atachagua tu chukulizi zinazofaa kutumika kulingana na muktadha wa tamko. Hivyo, msomaji atachagua chukulizi (i) kwa sababu ina kiwango cha juu cha uhusiano na inaleta maana kulingana na muktadha wa tamko na kuacha chukulizi (ii) kwa sababu haina kiwango cha juu cha uhusiano na haileti maana.

Msomaji ataweza kufahamu maana ya jamii kulingana na muktadha na kifaa cha uhusiano kuwa ina maana ya watu wenye asili moja wala si mkusanyiko wa watu au vitu. Vile vile, mhimili wa maana matini umetumika kuonyesha uhusiano wa kimaana katika sentensi. Ili

kufasiri maana ya kiwakilishi kiambata a- katika neno *akiongea*, msomaji atalazimika kurejelea nomino Bwana Kilonzo inayojitokeza katika sentensi hiyo.

**Urejelezi Nafsi**

Urejelezi nafsi umebainika kupitia matumizi ya viwakilishi nafsi huru, viwakilishi nafsi viambata, viwakilishi vimilikishi, vivumishi vimilikishi na viambishi ngeli.

**Viwakilishi Nafsi Viambata**

Urejelezi nafsi ulitumika katika *Habari za Kaunti* kupitia matumizi ya viwakilishi nafsi viambata. Kwa mfano:

*"Gavana wa Kaunti ya Lamu, Bw. Fahim Twaha, ameonya kuwa afisa yeyote ya umma atakayehusishwa na ufisadi atasimamishwa kazi."*

> *Akizungumza wakati wa kuapisha maafisa sita wapya wa Bodi ya Kuajiri wafanyakazi Kaunti ya Lamu (PSB), Bw. Twaha aliwasisitizia haja ya kuzingatia maadili, uwazi na uwajibikaji wakati watakapokuwa wakitekeleza majukumu yao.*

*"Alionya kwamba serikali yake haitamruhusu yeyote atakayejihusisha au kupatikana na kesi za ufisadi kuendelea kuhudumu katika bodi hiyo."*

*Ninawapongeza nyote kwa kufaulu kuchaguliwa. Langu ni kuwaomba kuzingatia maadili na kutekeleza majukumu yenu kwa uwazi na uwajibikaji. Ukijihusisha na ufisadi wa aina yoyote hutakuwa na budi ila kutemwa nje. Wakazi wa Lamu wanawategemea nyinyi ili kuleta sura mpya katika utekelezaji wa majukumu yenu, akasema Bwana Twaha.*

*Waliapishwa katika hafla maalum iliyoandaliwa kwenye makao makuu ya Kaunti ya Lamu mjini Mokowe iliyohudhuriwa pia na Naibu Gavana Abdulhakim Aboud… (Kazungu, 2020).*

Katika mfano huu, kiwakilishi nafsi kiambata *a-* katika neno *akizungumza* kimetumiwa kumrejelea Gavana wa Kaunti ya Lamu, *Bw. Fahim Twaha* ambaye alikuwa ametajwa katika aya ya kwanza. Kiwakilishi nafsi kiambata *a-* kimetumika kumrejelea kianafora *Gavana Twaha* na kuleta mshikamano katika matini. Ili msomaji afasiri maana ya kiwakilishi kiambata *a-* katika neno *akizungumza*, itambidi arejelee nomino *Gavana Twaha* iliyokuwa imetajwa katika matini.

Kiwakilishi nafsi kiambata *ni-* katika neno *ninawapongeza* kimetumika na mzungumzaji kujirejelea. Kiwakilishi nafsi kiambata *ni-* kinamrejelea mzungumzaji katika nafsi ya kwanza umoja. Mzungumzaji ni Gavana wa Kaunti ya Lamu ambaye alikuwa ametajwa katika aya zilizotangulia katika matini.

Kiwakilishi nafsi kiambata *u-* katika neno *ukijihusisha* kimetumiwa kiurejelezi kurejelea kila afisa aliyeajiriwa katika Bodi ya Kuajiri Wafanyikazi Kaunti ya Lamu. Kiwakilishi nafsi kiambata *u-* kinamrejelea mzungumzaji katika nafsi ya pili, umoja. Kila afisa miongoni mwa maafisa sita waliofaulu kuajiriwa katika Bodi ya Kuajiri Wafanyikazi Kaunti ya Lamu alikuwa akirejelewa. Maafisa sita hawa walikuwa wametajwa katika aya zilizotangulia. Urejelezi wa kianafora umetumika kubainisha maafisa wanaorejelewa na kuleta mshikamano katika matini.

Kiwakilishi nafsi kiambata *m-* katika neno *mtafaulu* kimetumika kuwarejelea maafisa sita waliofaulu kuajiriwa katika Bodi ya Kuajiri Wafanyikazi Kaunti ya Lamu. Kiwakilishi nafsi kiambata *m-* kinawarejelea wazungumziwa katika nafsi ya pili, wingi. Maafisa hawa walikuwa wametajwa awali katika matini. Urejelezi wa kianafora umetumika kuonyesha uhusiano wa kimaana na kuleta mshikamano katika matini. Mbali na matumizi ya viwakilishi nafsi viambata kianafora kuleta mshikamano, viwakilishi ngeli pia vimetumika kiurejelezi kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti*.

Viambishi ngeli vimetumiwa kuonyesha ngeli ya nomino inayorejelewa katika matini. Kiambishi *a-* katika maneno *akiongea* na *alionya* kinarejelea nomino *Gavana wa Kaunti ya Lamu, Bw. Fahim Twaha* ambayo ilikuwa imetajwa katika matini. Nomino inayorejelewa iko katika ngeli ya A-WA umoja kwa mujibu wa uainisho wa ngeli kwa kutumia viambishi vya upatanisho. Ili msomaji afasiri nomino inayorejelewa na kiambishi ngeli *A-*, atalazimika kurejelea nomino inayopatikana katika ngeli ya A-WA katika aya ya kwanza.

Kiwakilishi ngeli *WA-* katika neno *waliapishwa* kinarejelea nomino *maafisa* ambayo ilikuwa imetajwa katika matini. Nomino *maafisa* inapatikana katika ngeli ya A-WA, wingi. Ufasiri wa maana ya kiambishi *wa-* katika neno *waliapishwa* unategemea nomino *maafisa* ambayo ilikuwa imetajwa katika sehemu ya matini iliyotangulia. Kwa hivyo, viwakilishi ngeli huchangia kuleta mshikamano katika matini.

Mwandishi ametumia mhimili wa maana tambuzi kuelezea mambo yanayotendeka katika Kaunti ya Lamu. Ili msomaji afasiri maana ya neno Gavana, itambidi apanue maana ya neno Gavana kupitia dhana maalum ya kihali...
(i) mkuu wa jimbo
(ii) mtu anayeheshimiwa
(iii) mtu mwenye mamlaka
(iv) msimamizi wa Benki Kuu katika nchi fulani
(v) mwakilishi wa mfalme au malkia katika koloni

Chukulizi hizi zote zilizoorodheshwa hapo juu zinarejelea Gavana kwa jumla na zimehifadhiwa katika akili ya mwandishi na msomaji. Hata hivyo, chukulizi chache huweza kuchaguliwa na msomaji kurejelea Gavana. Msomaji atachagua chukulizi (i) hadi (iii) kwa sababu zina uhusiano wa hali ya juu kwa matini hii na zinaleta maana kwa ujumbe unaokusudiwa na mwandishi kwa msomaji. Chukulizi (iv) na (v) zitaachwa kwa sababu hazileti maana kulingana na muktadha wa tamko na hazina kiwango cha juu cha uhusiano. Chukulizi zilizokuzwa zinaweza kuchunguzwa kupitia dhana maalum ya kihali. Katika muktadha huu, dhana maalum ya kihali ya Gavana ni mkuu wa jimbo, anayeheshimiwa na mwenye mamlaka wala sio mwakilishi wa mfalme au malkia katika koloni au msimamizi wa Benki katika nchi fulani.

**Viwakilishi Nafsi Huru**

Viwakilishi nafsi huru vimetumika katika *Habari za Kaunti* kurejelea wazungumzaji na kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

*Wazee kutoka jamii ya Wakamba wamezidisha juhudi za kutaka Kiongozi wa Chama cha Wiper, Bw. Kalonzo Musyoka amrithi Rais Uhuru Kenyatta kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2022.*

*"Inatuhitaji sisi sote kukomesha siasa zisizokuwa na maana na kuelekeza nguvu zetu kumuunga Rais," alisema Bw. Kilonzo aliyesoma taarifa ya wazee hao…" (Muthini, 2020)*

Kiwakilishi nafsi huru *sisi* kimetumika na Bw. Kilonzo kuwarejelea kianafora *wazee kutoka jamii ya Wakamba* ambao walikuwa wameungana kuunga mkono nia ya Bw. Kalonzo Musyoka kumrithi Rais Uhuru Kenyatta baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2022. Kiwakilishi nafsi huru *sisi* kinaonyesha kuwa nomino inayozungumziwa ni ya nafsi ya kwanza, wingi. Ili kufasiri maana ya kiwakilishi nafsi huru *sisi*, msomaji atalazimika kurejelea neno *wazee* lililokuwa limetajwa katika aya ya kwanza. Kiwakilishi nafsi huru *sisi* kimetumika kianafora ili kuleta uhusiano wa kimaana na kuleta mshikamano katika matini.

Mhimili wa maana tambuzi umetumiwa kuelezea mambo ya urithi wa urais yanayojadiliwa na Wazee kutoka jamii ya Wakamba. Msomaji anaweza kufasiri maana ya neno *wazee* kwa kutumia mhimili wa kanuni tambuzi na mhimili wa kanuni mawasiliano. Neno hili limetumiwa na mwandishi kwa njia isiyo wazi kwa hivyo linaweza kufasiriwa na msomaji kwa kutumia kamusi ya ubongo. Itamlazimu msomaji apanue maana ya neno wazee kupitia kwa dhana maalum ya kihali. Kutokana na upanuzi huo, chukulizi zifuatazo zitakuzwa zinazohusiana na dhana ya wazee:
(i) watu
(ii) walioishi miaka mingi
(iii) watu wanaoheshimiwa
(iv) wanaume
(v) wazazi wa kiume

Chukulizi zote zilizoorodheshwa hapo juu zinarejelea wazee kwa jumla na zimehifadhiwa katika akili ya mwandishi na msomaji. Msomaji huteua tu chukulizi ambazo zinafaa kutumika kulingana na muktadha wa tamko. Hivyo basi, msomaji atachagua chukulizi (i) hadi (ii) kwa sababu zinaleta maana kulingana na muktadha wa tamko na zina uhusiano wa kiwango cha juu na kuacha chukulizi (iv) na (v) kwa sababu hazina uhusiano wa kiwango cha juu. Maana maalum itakayopatikana ya wazee ni watu walioishi miaka mingi wanaoheshimiwa wala sio wanaume au wazazi wa kiume hasa kina baba. Mwandishi ametumia mhimili wa maana matini kuonyesha uhusiano wa kimaana katika matini. Kwa mfano, ufasiri wa maana ya kiwakilishi nafsi huru *sisi* unategemea neno *wazee* kutoka jamii ya Wakamba ambao walikuwa wakihimizwa kukomesha siasa zisizokuwa na maana na kuelekeza nguvu zao kumuunga Rais Uhuru Kenyatta.

**Viwakilishi Vimilikishi**

Vimilikishi ni maneno yanayoeleza nomino inayomilikiwa na mtu. Vimilikishi huonyesha kitu au jambo linalomilikiwa na mtu. Viwakilishi vimilishi vimetumika katika *Habari za Kaunti* ili kuonyesha uhusiano wa kimaana na kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

"*Gavana wa Kaunti ya Lamu, Bw. Fahim Twaha, ameonya kuwa afisa yeyote ya umma atakayehusishwa na ufisadi atasimamishwa kazi."*

*"…Langu ni kuwaomba kuzingatia maadili na kutekeleza majukumu yenu kwa uwazi na uwajibikaji. Ukijihusisha na ufisadi wa aina yoyote hutakuwa na budi ila kutemwa nje…" (Kazungu, 2020).*

Kiwakilishi kimilikishi *langu* kimetumika kianafora na mzungumzaji kujirejelea. Gavana Twaha alikuwa akitoa ombi lake kwa maafisa sita waliofaulu kuchaguliwa kuhudumu katika Bodi ya Kuajiri Wafanyakazi Kaunti ya Lamu. Ufasiri wa maana ya kiwakilishi kimilikishi *langu* unategemea nomino Gavana wa Kaunti ya Lamu, Bw. Fahim Twaha iliyokuwa imetajwa katika aya iliyotangulia. Mhimili wa maana matini umetumika kuleta mshikamano katika matini.

Ili msomaji afasiri maana ya kiwakilishi kimilikishi *langu*, atambidi arejelee nomino Gavana wa Kaunti ya Lamu, Bw. Fahim Twaha iliyokuwa imetajwa katika aya iliyotangulia. Mhimili wa maana tambuzi umetumika kueleza kuhusu ufisadi unaoendelezwa na maafisa wanaofanya kazi katika Kaunti ya Lamu. Mwandishi ametumia neno ufisadi kwa njia iliyo wazi; msomaji anaweza kupata maana ya ufisadi kwa kufasiri moja kwa moja maana iliyosimbwa katika neno hilo. Msomaji atapata kuwa neno ufisadi lina maana ya kila aina ya uovu.

**Urejelezi wa Kuashiria**

Urejelezi wa kuashiria huonyesha mahali ambapo mtu, jambo au kitu kipo kwa mkabala wa mzungumzaji. Urejelezi wa kuashiria umetumika katika *Habari za Kaunti* ili kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano:

*"Watu wawili wenye akili taahira wanashughulikiwa na shirika moja la kutoa msaada baada ya kubainika kuambukizwa maradhi ya virusi vya Corona katika mtaa wa Majengo, Mombasa."*

*"Wawili hao ni miongoni mwa wagonjwa wengine 15 wenye akili punguani waliochukuliwa kutoka maeneo mbalimbali kutoka kaunti hiyo mwezi iliyopita katika kaunti hiyo mwezi uliopita."*

*"Akizungumza na Taifa Leo, Mwenyekiti wa shirika la Women Empowerment Network ambaye amekuwa akishughulikia na kupigania haki za wagonjwa wa akili katika kaunti hiyo, alisema walipokea matokeo hayo baada ya kaunti kuwapima watu hao 15…" (Mutheu, 2020).*

Watu wawili wenye akili timamu ambao walikuwa wameambukizwa virusi vya Corona katika mtaa wa Majengo, Mombasa wamerejelewa kianafora kupitia matumizi ya kivumishi kiashiria *hao*. Vilevile, watu 15 kutoka maeneo mbalimbali kutoka Kaunti ya Mombasa waliopimwa kuchunguzwa kama walikuwa na virusi vya Corona wamerejelewa kianafora kupitia matumizi ya kivumishi kiashiria *hao*. Kaunti ya Mombasa imerejelewa kianafora kupitia matumizi ya kivumishi cha kuashiria *hiyo*.

Mhimili wa maana tambuzi umetumiwa kuelezea mambo yanayotendeka katika Kaunti ya Mombasa. Neno taahira limetumika kwa maana tambuzi. Mwandishi ametumia neno taahira kwa njia isiyo wazi. Ili kufikia maana ya neno taahira, itambidi msomaji kupanua maana neno taahira kwa kutumia kamusi ya ubongo wake ili kukuza chukulizi zifuatazo ya dhana taahira:

(i) kuchelewa
(ii) mtu asiyekuwa na akili razini

Chukulizi hizi mbili zilizoorodheshwa zinarejelea neno taahira kwa jumla na zimehifadhiwa katika akili ya msemaji na msikilizaji. Msomaji atachagua tu chukulizi zinazofaa kutumika kulingana na muktadha wa tamko na kiwango cha uhusiano. Chukulizi (ii) itachaguliwa ilhali chukulizi (i) itaachwa. Chukulizi (ii) inaleta maana na ina kiwango cha juu cha uhusiano ilhali chukulizi (i) itaaachwa kwa sababu haina maana na haina kiwango cha juu cha uhusiano. Msomaji ataweza kuelewa kulingana na muktadha na kifaa cha uhusiano kuwa taahira ina maana ya mtu asiyekuwa na akili razini wala sio kuchelewa.

Mhimili wa maana matini umetumiwa kuleta mshikamano katika matini. Kwa mfano, kivumishi *hao* katika aya ya pili kinawarejelea *watu wawili wenye akili taahira* waliokuwa wametajwa katika aya ya kwanza. Ili kuelewa maana ya kivumishi *hao*, *hiyo* na *hayo* itambidi msomaji arejelee *watu wawili wenye akili taahira*, *Kaunti ya Mombasa* na *matokeo* ya wagonjwa 15 wenye akili punguani waliochukuliwa waliokuwa wametajwa awali katika matini.

**Urejelezi wa Kulinganisha**

Urejelezi wa kulinganisha hutumiwa kuonyesha hali ya kufanana au kutofanana kwa vitu viwili au zaidi. Urejelezi huu, ukilinganishwa na urejelezi nafsi na urejelezi wa kuashiria haujatumika sana katika *Habari za Kaunti*. Kwa mfano:

> *Viongozi watatu wa chama cha ODM wamekanusha madai kuwa mageuzi ya kikatiba yanayotarajiwa kutekelezwa chini ya ripoti ya Mpango wa Maridhiano (BBI), yanalenga kubuni nafasi za kisiasa kwa viongozi wanaoshindwa kwenye uchaguzi.*

*"Watatu hao ni Kiongozi wa Wachache kwenye Seneti, Seneta James Orengo, Seneta Moses Kajwang' (Homa bay) na mbunge Otiende Amollo (Rarieda)."*

> *Viongozi wanaoendesha kampeni za kuipinga ripoti wanapaswa kukoma. Tunataka Kenya kuwa na amani hata baada ya uchaguzi. Hili linaweza tu kufanikishwa kupitia mageuzi ya kikatiba yaliyojumuishwa kwenye ripoti. Mpango huo ni kama gari la moshi ambalo haliwezi kusimamishwa na yeyote," akasema Bw. Kajwang… (Odiwuor, 2020).*

Katika mfano huu, mpango wa BBI unalinganishwa na gari la moshi kama inavyodhihirika katika sentensi '*Mpango wa BBI ni kama gari la moshi ambalo haliwezi kusimamishwa na yeyote…*' Msemaji anamaanisha kuwa mpango wa BBI hauwezi kusimamishwa na mtu yeyote kwa sababu ulikuwa umeanza. Urejelezi wa kulinganisha haujatumika sana katika *Habari za Kaunti* kwa sababu hauchangii sana katika kuleta mshikamano katika matini ukilinganishwa na urejelezi nafsi na urejelezi wa kuashiria. Mhimili wa maana tambuzi umetumika kueleza mambo yanayohusiana na Mpango wa Maridhiano. Mpango huu umelinganishwa na gari la moshi. Neno gari la moshi limetumika kwa maana tambuzi. Neno hili limetumika kwa njia iliyo wazi. Msomaji atafasiri maana ya neno gari la moshi kwa kutumia mkakati wa kubana. Katui (2026) anaeleza kuwa ubanaji ni ule mchakato wa kutumia neno au kirai kuashiria dhana mahususi zaidi ya maana iliyosimbwa kiisimu.Katika mfano huu, msomaji atafasiri moja kwa moja maana iliyosimbwa katika neno gari la moshi. Msomaji atakuwa na sifa zifuatazo zinazorejelea dhana ya gari la moshi akilini mwake:
(i) gari refu
(ii) linatumia reli
(iii) linaendeshwa kwa kasi
(iv) linasimama katika vituo fulani
(v) linatoa moshi

Sifa hizi zote zinarejelea gari la moshi kwa jumla. Msomaji atachukua sifa zote zilizoorodheshwa hapo juu kurejelea dhana ya gari la moshi. Maana ya kihali inayopatikana kutokana na muktadha wa tamko ni kuwa Mpango wa Maridhiano, kama gari la moshi linaloendeshwa kwa kutumia reli kwa kasi na kutoa moshi, haliwezi kusimamishwa na mtu yeyote bali litasimama tu katika kituo fulani au mwishoni mwa safari.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho**: Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kubainisha aina za urejelezi katika gazeti la *Taifa Leo.* Utafiti huu umeonyesha kwamba urejelezi wa kiendofora (anafora na katafora), urejelezi nafsi na urejelezi wa kuashiria umetumika katika *Habari za Kaunti* ili kuleta mshikamano katika matini. Urejelezi nafsi hubainika katika matini kupitia matumizi ya viwakilishi nafsi huru, viwakilishi nafsi viambata, viwakilishi ngeli, viwakilishi vimilikishi na vivumishi vimilikishi.

Makala hii imeonyesha kuwa vivumishi viashiria vimetumika kiurejelezi ili kuleta mshikamano katika matini. Imebainika kuwa vivumishi viashiria hufanya kazi ya kuonyesha kama kitu au mtu yuko karibu, mbali kidogo (wastani) au mbali sana. Aidha, Makala hii imeonyesha kuwa urejelezi wa kulinganisha haujatumika sana kuleta mshikamano katika matini ikilinganishwa na urejelezi nafsi na urejelezi wa kuashiria. Urejelezi wa kulinganisha umedhihirika kupitia matumizi ya maneno ya kulinganisha kama vile *sawa na* pamoja na *kama*. Isitoshe, mihimili ya kanuni tambuzi na kanuni mawasiliano ya nadharia ya Uhusiano imebainisha kuwa urejelezi wa kiakili unaweza kutumika kuleta mshikamano kupitia urejelezi wa muktadha, ufahamu wa awali na kiwango cha uhusiano. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa urejelezi ni kiungo muhimu katika kuleta mshikamano na kufanikisha mawasiliano ya kimaana.

**Mapendekezo**: Utafiti wetu umejikita katika kuchunguza aina za urejelezi zilizotumika kuleta mshikamano katika *Habari za Kaunti* katika gazeti la *Taifa Leo*. Tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusu matumizi ya urejelezi kuleta mshikamano katika *Tahariri* katika gazeti la *Taifa Leo*. Kwa kufanya hivi, utafiti huu utabainisha aina za urejelezi zinazotumiwa waandishi wa tahariri ili kuleta mshikamano katika matini zao na kufanikisha mawasiliano.

**MAREJELEO**


Carston, R. (2002). *Thoughts and utterances: The pragmatics of explicit communication*. Blackwell.

Habarkah, S. (2019). *An analysis of textual personal reference in English version of Open Letter to Baghdadi* (Strata One thesis). State Islamic University Jakarta.

Halliday, M. A. K. (1985). *An introduction to functional grammar*. Edward Arnold.

Halliday, M. A. K. (1994). *An introduction to functional grammar* (2nd ed.). Edward Arnold.

Halliday, M. A. K., & Hasan, R. (1976). *Cohesion in English*. Longman.

Halliday, M. A. K., & Matthiessen, C. (1999). *Construing experience through meaning: A language-based approach to cognition*. Edward Arnold.

Halliday, M. A. K., & Matthiessen, C. (2004). *An introduction to functional grammar* (3rd ed.). Arnold.

Katui, S. P. (2026). Uchanganuzi wa ubanaji wa maana za maneno katika jukwaa la Facebook. *Journal of Kiswahili and Other African Languages, 4*(1), 13–23. https://doi.org/10.58721/jkal.v4i1.1591

Kazungu, K. (2020, June 8). Gavana aonya maafisa wake kuhusu ufisadi. *Taifa Leo*.

Khofidoh, N. (2017). *Anaphoric and cataphoric function on personal references used in English political news articles* (Unpublished master's thesis). State Institute for Islamic Studies (IAIN) Salatiga.

Matthiessen, C. (2013). *Introduction to functional grammar*. Routledge.

Mutheu, D. (2020, June 4). Shirika lasaidia watu wenye akili taahira. *Taifa Leo*.

Mutheu, D. (2020, June 9). Serikali yatetea ubomoaji Pirates. *Taifa Leo*.

Muthini, S. (2020, June 10). Wazee waunga mkono azma ya Kalonzo kumrithi Uhuru. *Taifa Leo*.

Odiwuor, G. (2020, July 12). BBI si njama kufaidi watakaokosa viti. *Taifa Leo*.

Ojode, J. O. (2014). *Uchanganuzi wa sitiari katika nyimbo za Taarab: Mfano wa Mzee Yusuf na Mwanahawa Ally, Unguja* (Unpublished master's thesis). Chuo Kikuu cha Kisii.

Saddimbah, C. R. (2011). *Cohesive devices in Dholuo sermons: A textual analysis* (Unpublished master's thesis). Kenyatta University.

Schubert, C. (2008). *Englische Textlinguistik: Eine Einführung*. Schmidt.

Sperber, D., & Wilson, D. (1995). *Relevance: Communication and cognition* (2nd ed.). Blackwell.

Sperber, D., & Wilson, D. (2004). Relevance theory. In L. R. Horn & G. Ward (Eds.), *The handbook of pragmatics* (pp. 607–632). Blackwell.

Sukthanker, R., Poria, S., Cambria, E., & Thirunavukarasu, R. (2020). Anaphora and coreference resolution: A review. *Information Fusion, 59*, 139–162. https://doi.org/10.1016/j.inffus.2020.01.010

Toews, N. (2016). *Relevance theory and proverbs: Exploring context through explicatures and implicatures* (Unpublished master's thesis). Trinity Western University.

Wilson, D. (2003). Relevance theory and lexical pragmatics. *Italian Journal of Linguistics, 15*, 273–291.

Wilson, D., & Sperber, D. (2002). Truthfulness and relevance. *Mind, 111*(443), 583–632. https://doi.org/10.1093/mind/111.443.583